**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU 31 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2017/2018

Ofisi ya Bunge,
Idara ya Kamati za Bunge,
**DODOMA**

April, 2017

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU 31 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2017/2018**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Fungu 31 kwa Mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,**pamoja na nia nzuri ya Serikali katika kudhibiti kasi ya uharibifu wa mazingira na athari za mabadiriko ya tabianchi bado jitihada za ziada zinahitajika. Shughuli za kibinadamu ndicho chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira ikiwemo shughuli za Kilimo na Ufugaji usiozingatia taratibu; uvunaji wa misitu usiozingatia taratibu; na uvuvi haramu. Kwa muktadha huu Serikali inatakiwa kuchukua hatua za makusudi za kusimamia na kuhifadhi mazingira kwani kukwepa gharama za kutunza mazingira ni kukaribisha janga kwa nchi yetu na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017, kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kujadiri Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi

ya Makamu wa Rais Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuchambua Mpango na Bajeti kwa mwaka fedha wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2016/2017 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi. Katika kufanya Uchambuzi Kamati ilitumia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Taarifa ya ziara kwenye Miradi na mahojiano wakati wa vikao.

#### 2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Rais haikuwa na makusanyo ya Maduhuli.

### 2.1.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha **2016/2017** Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **20,386,699,448.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **9,413,616,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **10,973,083,448.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika shilingi **9,413,616,000.00**ambazo nibajeti ya matumizi ya kawaida Shilingi **2,846,299,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishina na Shilingi **6,567,317,000.00** ni za matumizi mengineyo. Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa Shilingi **2,314,680,000.00** ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) na kiasi kinachosalia Shilingi **4,252,637,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo(OC) katika Idara na Vitengo vya Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha za miradi ya maendeleo Shilingi **10,973,083,448**.00 zilizoidhinishwa, Shilingi **8,000,000,000.00**ni fedha za ndani na Shilingi **2,973,083,443.00** ni fedha za nje.

**Fedha zilizopokelewa hadi 15 Machi, 2017**

**Mheshimiwa Spika,**kati ya Shilingi **20,386,699,448.00**zilizoidhinishwa kwa ajiliya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, ni Shilingi **7,793,493,737.18** tu ndizo zilikuwa zimetolewahadi kufikia 15 Machi, 2017. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **38.2**ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,**Kati ya Shilingi **9,413,616,448.00** zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni Shilingi **6,555,916,168.68**tu ndizo zilizokuwazimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **69.9**ya fedha zote

zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida Shilingi**1,905,596,990.00**ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **2,964,514,853.84** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo(OC). Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa Shilingi **51,040,660.00**zililipa madeni ya watumishi, Shilingi **177,093,664.84** zililipia madeni ya wazabuni na Shilingi **1,457,670,000.00** ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kiasi kinachosalia kwaajili ya uendeshaji wa Ofisi ni Shilingi **1,278,710,526.00** ambazo hazikukidhi mahitaji halisi.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Shilingi **10,973,083,448.00** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ni Shilingi **1,237,577,568.50** tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia **11.3** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Aidha kati ya Shilingi **8,000,000,000.00** za bajeti ya fedha za ndani ni Shilingi **236,186,455.00** tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia **2.9** ya bajeti yote ya fedha za ndani na Shilingi **2,973,083,443.00** za bajeti ya fedha za nje ni **1,001,391,113.50** tundizo zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia **33.6** ya bajeti yote ya fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida umeonekana kuwa wakuridhisha kwa kuwa unachangiwa na fedha za mishahara ambazo hutolewa kila mwezi. Katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira, upatiakanajiwa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha hivyo kupelekea kukwamisha utekelezaji wa mipangoya Wizara.

## 2.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** jedwali lifuatalo linaonyesha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 na upatikanaji wa fedha.

| **Mradi Na.** | **Jina la Mradi** | **Fedha zilizoidhinishwa 2016/17** | | **Fedha zilizotolewa hadi tarehe 15 Machi, 2017** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Fedha za Ndani Sh. | Fedha za Nje Sh. | Fedha za Ndani Sh. | Fedha za Nje Sh. |
| 5301 | Climate Change Adaptation Programme | 3,200,000,000 | 2,694,633,448 | 0 | 911,151,113.5 |
| 5304 | Ozone Depleting Substances Project | 80,000,000 | 147,000,000 | 0 | 0 |
| 5305 | Stockholm Convention Implementation Project | 120,000,000 | 131,450,000 | 0 | 90,240,000.0 |
| 5307 | The National Environmental Trust Fund | 2,100,000,000 | 0 | | |
| 6309 | Construction of VP Office and Residence in Znz | 700,000,000 | 0 | 236,186,455 | 0 |
| 6389 | Construction and of VP Office Luthuli & Rehabilitation of State Lodges | 700,000,000 | 0 | | |
| 6569 | Lake Tanganyika Env. Mng. Programme | 600,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| 6571 | EMA Implementation Support Programme | 500,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **8,000,000,000** | **2,973,083,448** | **236,186,455** | **1,001,391,113.5** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika bajeti ya 2016/2017 kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, iliidhinishiwa shilingi **5,894,633,000.00** kwa ajili ya Mradi namba 5301 wa *Climate Change Adaptation Programme* ambao ni mradi wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Maeneo ya mradi huu ni Ocean Road, Kigamboni, Pangani, Kisiwa Panza (Pemba) na Kilimani Unguja.Hata hivyo kwasababu ya ufinyu wa muda Kamati ilifanikiwa kutembelea na kujionea hali ya utekelezaji wa Mradi huu katika eneo la Pangani na Ocean Road.

### 2.2.2 Mradi wa Mabadaliko ya Tabianchi

**Mheshimiwa Spika**, mabadiriko ya tabianchi yamesabisha kuongezeka kwa usawa wa bahari (sea level rise) kwa sentemita **19** katika kipindi cha miaka **50** iliyopita. Ongezeka la usawa wa bahari linachangia uharibifu wa mwambao wa Pwani, na kutoweka kwa baadhi ya visiwa kama; Panza Zanzibar, Maziwa Pangani, Fungu la Nyani Rufuji, na baadhi ya visima vya maji baridi katika maeneo ya Bagamoyo kuharibiwa na maji chumvi. Maisha ya wananchi wanaoishi katika mwambao wa Bahari ya Hindi na kutegemea Bahari yapo hatarini kutokana na kumomonyoka kwa fukwe na upotevu wa viumbe baharini.

**i) Ujenzi wa Ukuta wa Pangani**

Ujenzi wa Ukuta wa mto Pangani unajumuisha urefu wa meta 950 kwa upande wa Kaskazini yaani Pangani Mjini na meta 660 upande wa Bweni. Ujenzi wa ukuta huu ulianza rasmi tangu tarehe 01Machi, 2017, Mkandarasi aliyepewa kazi hii ni DEZO Civil

Contractors. Mradi huu unakisiwa kuwa utagharimu kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni mpaka utakapokamilika. Mradi unatekelezwa kwa fedha za wafadhili kwa asilimia **90,** kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni ambazo zimekwishatolewa kwa upande wa Pangani Mashariki, wakati asilimia **10** ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu kwa upande Pangani Magharibi bado hazijatolewa.Mradi huu unatarajiwa kukamilika Novemba, 2017 iwapo mipango yote itakwenda kama iliyopangwa.

**CHANGAMOTO**

**Mheshimiwa Spika,**Mradi huu unakabiliwa na Changamoto kuu tatu kama ifuatavyo:-

- Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa ukuta wa mto wa Pangani kumecheleweshа juhudi za kuanza mchakato wa kuanza upembuzi yakinifu kwa upande wa PANGADECO;
- Kuendelea kuharibika kwa eneo la PANGADECO ambapo hali ni mbaya na eneo hili la ufukweni mwa mji wa Pangani ni hatarishi kwa maisha ya wanadamu kwahiyo zinahitajika juhudi mahususi ili kukabiliana na athari hizo.
- Upande wa Pangani Mashrariki mradi unatekelezwa kwa fedha za Wafadhili hivyo utekelezaji wake unaendelea. Katikaupande waPangani Magharibi mradi unatekelezwa kutokana na fedha za ndani. Serikali bado haijapeleka fedha ilizotenga hivyo kucheleweshа utekelezaji na uharibufu kuongezeka kwa kadri siku zinavyokwenda.

**ii) Ujenzi wa Ukuta wa Ocean Road**

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa eneo la *Ocean Road.* Hali ya utekelezaji wa Mradi inaendelea vizuri Mkandarasi amekwisha anza kazi baada ya kupata

fedha za wafadhili kutoka*Adaptation Fund*. Kamati inapongeza hatua ya Wizara ya kuamua kutafuta wafadhirina kuutekeleza mradi huu kwa haraka. Kwani utekelezaji wa mradi huu utasaidia kukabiliana na kupungua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi yanayosababisha ongezeko la kina cha Bahari yetu.

### 2.2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/207

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilishauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa Mazingira kwa kutenga fedha za kutosha lakini pia fedha hizo zitolewe kwa wakati. Kwa Mfano Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2017 ilikuwa hajiapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo jambo linalokwamisha utekelezaji wa Miradi hiyo.

i) Kamati inaishauri Serikali kuwa pamoja na nia yake nzuri ya kusimamia uhifadhi wa Mazingra nchini, iangalie namna ya kuongeza bajeti ya Mazingira. Jambo hili litawezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira na kupunguza uhitaji wa fedha nyingi zinazotumika katika kurekebisha miundombinu za kimazingira na uoto wa asili. **(usipoziba ufa utajenga ukuta);**

ii) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa jitihada wanazozifanya za kutafuta wahisani ili kulinusura Taifa na janga la uharibifu wa mazingira. Kamati inawaomba waendelee na juhudi za kutafuta fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali ilikuongezea kwenye fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya bajeti ya mazingira; na

iii) Katika mradi wa Pangani Serikali ipeleke fedha za bajeti ya ndani asilimia **10** ya fehda zote za mradiili utekelezaji usikwame.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo nane (8). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii;

i) ***Serikali ianze kutekeleza ujenzi wa vituo vya kupumzikia wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini haraka iwezekanavyo***. Agizo hili lilikuwa miongoni mwa maagizo ya kamati katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 na kwa mwaka huo wa fedha Serikali ilifanikiwa kujenga kituo kimoja tu katika Wilaya ya Mufindi Mkoani Iringa. Agizo hili liliendelea kusisitizwa na Kamati na kuwa miongoni mwa maagizo ambayo yatatekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Maelezo ya Serikali kuhuusu utekelezaji wake ni kuwa, Ofisi inaendelea kuhamasisha wadau wa mazingira na sekta binafsi kujenga vituo hivyo. Pia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetambua maeneo ya ujenzi wa vituo hivyo katika mpango wa ujenzi wa barabara kuu. Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa agizo hili, pia inaitaka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kubainisha kuwa imebaini uhitaji wa Vituo vingapi na ujenzi utaanza lini kuazia sasa.

ii) ***Bajeti ya kuendeleza upandaji wa miti iongezwe. Aidha vyanzo vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira vitokane pia na Wizara nyingine. Vyanzo hivyo***

***vitambuliwe na kuhamishiwa katika Mfuko.*** Serikali ilitoa maelezo kuwa zoezi la upandaji miti linafanya na kila wilaya na kusimamiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambapo kila wilaya hutakiwa kupanda miti **1,500,000** kila mwaka. Kamati na inaamini kuwa miti **1,500,000** ni miti mingi sana kiasi kwamba kama ingekuwa imepandwa tayari athari (impact) yake ingekuwa imeonekana. Kamati inashauri agizo hili litekelezwa kwa haraka na baada ya kupandwa kuwa na ufuatiliaji kuhakikisha inakua.

**Mheshimiwa Spika,**kwa upande wa Mfuko wa Mazingira Kamati ilielezwa kwamba usimamizi wa Mazingira kwa kipindi cha 2016/2017 Serikali imezindua rasmi Mfuko wa Mazingira  na Bodi ya wadhamini wa Mfuko imezinduliwa. Mapendekezo ya vyanzo vya Mapato vya Mfuko kutoka sekta nyingine yamewasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikia lakini iongeze kasi ya utekelezaji.  Kamati inaamini kwamba kupatikana kwa Mfuko huu kutarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa RaisMazingira na kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, **Fungu 31** hakuna mapato yatakayokusanywa.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi kwa ujumla wake na kubaini kuwa Mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati haikuridhishwa na ukomo wa Bajeti unaopitishwa kwa ajili ya Ofisi hii kwakuwa haiendani na umuhimu wa Ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha **2017/2018** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inaomba kuidhinishiwa Shilingi **15,002,988,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha zinazoombwa Shilingi **10,634,020,440.00**ni kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, ambapo Shilingi **6,788,452,437.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida Shilingi **2,215,044.000.00**ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia Shilingi **1,630,524,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi cha ruzuku kinacho ombwa kwa ajili ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni Shilingi **2,215,044.000.00.** Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **4.3** ikilinganishwa na Shilingi **2,314,680,000.00** bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha **2017/2018** Idara ya Mazingira imepangiwa jumla ya shilingi **3,845,568,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.Kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia **5.5** ikilinganishwa na Shilingi **3,647,654,000.00** bajeti inayotekelezwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa kwa ajili Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kwa kwa ajili ya miradi ya maendekeo kwa mwaka wa

fedha**2017/2018** ni Shilingi **6,788,452,437.00.**Kiasi hiki nipungufu kwa asilimia **38**ikilinganishwa na Shilingi **10,973,083,448.00** zilizoidhinishwa mwaka wa fedha **2016/2017**. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,000,000,000.00**ni fedha za ndani na Shilingi **3,788,452,437.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Raisi inaendelea kufanya mawasiliano na washirika wa maendeleo ambao wameonesha nia ya kusaidia katika maeneo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya kemikali. Ofisi pia imekamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira. Mapendekezo haya yatawasilishwa katika ngazi husika kwa ajili ya maamuzi na utekelezaji.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 HALI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, idadi ya Watanzania kwa sasa inakisiwa kuwa milioni **51**, ambapo inakisiwa kuwa kuna ongezeko la asilimia **2.7** kwa mwaka, na kuwa kutakuwa na watu milioni **100** ifikapo mwaka **2035.** Ongezekohili linaashiria ongezeko la mahitaji ya rasimali za asili hasa ardhi na misitu.

**Mheshimiwa Spika**, asilimia **90** ya nishati inayotumika nchini inatokana na misitu na hii inachangia upotevu wa misitu yetu kwa asilimia **70**. Mfano Dar es Salaam peke yake hutumia magunia **200,000-300,000** (yenye wasitani wa kilo **50**) kila moja kwa mwezi ambayo kwa mwaka ni sawa na tani laki tano **(500,000).** Aidha, Wastani wa matumizi ya magogo/kuni kwa mtu mmoja kwa mwaka ni wastani wa mita moja ya ujazo **(1m)** ambayo ni takribani mita za ujazo milioni **50**za magogo kwa mwaka

kwanchi nzima. Madhara ya ufyekaji wa misitu ni pamoja na uharibifu wa mazingira inaharibu mifumo ya hewa na kusababisha mabadiriko ya tabianchi vilevile upungufu wa mvua.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mwenendo wa uharibifu wa mazingira nchini zinahitajika jitihada za mahsusi za kuhifadhi mazingira. Hatua ambayo itaepusha gharama kubwa zinazotumika kurekebisha miundombinu mbalimbali ya kimazingira katika nchi yetu (mfano mikondo na maporomoko ya maji).

## 5.2 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** suala la uhifadhi wa Mazingira ni suala mtambuka hata hivyo linazihusu zaidi Wizara tatuMaliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira na Wizara ya Kilimo na Mifugo ambapo imeonekena kuwa na muingiliano wa sheria.Kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kunamuingiliano katika sheria za misitu. Ambapo Wizara ya Maliasili na utalii misitu ni chanzo cha mapato, na Wizara ya Kilimo ya Mifugo inatumia misitu kama maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo wakati Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inasimamia katika kuhifadhi misitu.Kamati inaishauri Serikalikuziangalia upya sheria zetu na kuhamasishaWizara hizi zifanye kazi kwa pamoja kwa manufaa ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia **5** ziingie katika mfuko wa mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta, tozo ya magogo n.k;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mazingira nchini ipo lakini haijasimamiwa ipasavyo katika maeneo mengi nchini hivyo kundelea kushamiri kwa uharibifu wa Mazingira. Kamati inaishauiri Serikali kusimamia Sheria hiyo kikamilifu ili kulinusuru Taifa letu na kupunguza uwezekano wa kukumbwa na mabadiriko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada za upandaji miti aina ya mikoko katika mwambao wa bahari ya Hindi, pia udhibiti wa ukataji haramu wa mikoko unaofanywa na wananchi waishio katika mwambao wa bahari ya Hindi uimarishwe;

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingi ya mazingira haikufanikiwa kutokana na ushirikishwaji mdogo wa jamii katika utekelezaji wake. Mfano mradi wa upandaji miti na mradi wa kukabiliana na mabadiliki ya tabianchi, wakati Serikali inasisitiza upandaji wa miti wananchi wamekuwa wakivuna miti bila utaratibu maalumu hivyo kusababisha majanga. Kamati inaishauri serikali iendelee kukuza uelewa kwa jamii kwa kuwashirikisha kikamilifu katika kutekeleza miradi yake ya mazingira;

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la watu linalokadiriwa mpaka kufikia 2035 linaashiria ongezeko kubwa la uhitaji wa rasilimali hususani misitu kwa ajili ya nishati. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati wa makusudi wa kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya utumiaji wa teknolojia za nishati mbadala (majiko bunifu na umeme wa jua) ili kupunguza uvunaji wa misitu kwa ajili ya nishati. Mkakati huu uweze kumsaidia mwananchi kuyatunza mazingira wakati huohuo anapata nishati mbadala kwa bei nafuu;

**Mheshimiwa Spika**, Mazingira ni suala mtambuka lakini katika Wizara na Idara za Serikali hakuna kifungu cha bajeti ambacho kinatengewa

fedha kwa ajili ya masuala yanayohusu mazingira. Hapo awali vifungu hivi vilikuwepo katika bajeti za Wizara zote ila viliondolewa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuwa katika bajeti za Wizara, Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini kuwe na kifungu cha bajeti ya Mazingira;

**Mhesimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza suala la Serikali kukutana na wadau wa plastiki na kufanya mazungumzo ili kupata muafaka wa namna ya kusitisha utengenezaji wa bidhaa za plastiki bila kuathiri ajira na uwekezaji uliofanyika. Seriakali itoe muda wa kutosha kwa wadau kuhamia katika teknolojia itakayowawezesha kuzalisha plastiki rafiki kwa mazingira ambazo pindi zitakapo kutana na jua na mvua zitaoza kwa haraka. Serikali iongeze nguvu katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari za uharibifu wa mazingira na umuhimu wa utunzaji wa mazingira; na kuhimiza uanzishwaji wa Viwanda vinavyotumia taka za plastiki kama malighafi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba suala mazingira linazungumzwa sana na viongozi wa Serikali, viongozi wa dini na Asasi mbalimbali za kiraia lakini halijapewa umuhimu unaostahili na Serikali yetu. Kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya mazingira katika Mikoa na Halmashauri zetu jambo linalosababisha ugumu katika kupambana na janga hili. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya ajira za maafisa mazingira katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Hatua hii itasaidi katika utekelezaji wa masuala yanayohusu mazingira.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kukamilisha taarifa hii. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb | Mwenyekiti |
| (ii) | Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) | Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) | Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) | Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) | Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) | Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) | Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) | Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) | Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) | Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) | Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) | Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| (xiv) | Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb | Mjumbe |
| (xv) | Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | Mjumbe |
| (xvi) | Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | Mjumbe |
| (xvii) | Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | Mjumbe |
| (xviii) | Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb | Mjumbe |
| (xix) | Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb | Mjumbe |
| (xx) | Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | Mjumbe |
| (xxi) | Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb | Mjumbe |
| (xxii) | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| (xxiii) | Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb | Mjumbe |
| (xxiv) | Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| (xxv) | Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb | Mjumbe |
| (xxvi) | Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb | Mjumbe |
| (xxvii) | Mhe. Joyce John Mukya, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais Mungano na Mazingira, Mhe.January Y Makamba, Mbna Naibu wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina, MbMakatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni kiasi cha Shilingi **15,002,988,437.00**.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe.Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

24Aprili, 2017